JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**


Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: **ps@mit.go.tz**
Tovuti: **www.mit.go.tz**

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
**40478 DODOMA**.


## TAARIFA KWA UMMA

## 1. UTANGULIZI

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kama tunavyofahamu Wizara ya Viwanda na Biashara inatekeleza jukumu la kufanya tathmini na kuratibu ukusanyaji wa takwimu za mwenendo wa bei za mazao ya chakula na bidhaa muhimu nchini. Kutokana na umuhimu wa taarifa hizi kutumiwa na wafanya maamuzi, wazalishaji, wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla, Wizara inaendelea kuutaarifu Umma kuhusu tathmini ya bei hizo. Vilevile, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali na stahiki katika kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa muhimu nchini.

Leo napenda kuwaletea uchambuzi wa mwenendo wa bei za bidhaa muhimu kwa mwaka 2022/2023, yaani kwa kipindi kilichoanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.

## 2. MWENENDO WA BEI ZA MAZAO NA BIDHAA ZA VYAKULA

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Uzalishaji wa mazao muhimu ya chakula nchini kwa mwaka 2021/2022 ulikuwa ni takribani tani milioni 17.15 ikiwa ni pungufu kwa tani milioni 1.52 ukilinganisha na uzalishaji wa mazao hayo kwa mwaka 2020/21. Mazao muhimu yanayotajwa hapa ni pamoja na mahindi, mchele, ngano, mtama, uwele, ulezi, mihogo, maharage na mikunde, ndizi na viazi. Kupungua huko kwa uzalishaji kulisababishwa na mtawanyiko wa unyeshaji wa mvua usioridhisha. Katika taarifa hii ya mwaka ya mwenendo wa bei za mazao na bidhaa za vyakula, tutaangalia mazao ya mahindi, mchele, maharage, ngano na viazi mviringo. Bidhaa nyingine za vyakula tukavyochambua ni unga wa mahindi, unga wa ngano pamoja na mafuta ya kupikia.

## i. Mahindi

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Uzalishaji wa mahindi kwa mwaka 2021/2022 ulikuwa ni tani milioni 6.417 ambazo zilikuwa pungufu kwa tani 620,000 ukilinganisha na uzalishaji wa mwaka 2020/2021 uliokuwa tani milioni 7.039. Sehemu ya kiasi hicho cha mahindi kilichozalishwa katika mwaka 2021/2022 ndicho kilichoingia katika msimu wa masoko ya mazao wa mwaka 2022/2023. Hivyo, ni dhahiri kuwa ugavi wa mahindi kwa mwaka 2022/2023 uliathirika kutokana na kupungua kwa uzalishaji na hivyo kusababisha bei ya mahindi kwa walaji kuwa ya juu.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 wastani wa bei ya chini ya mahindi ilikuwa ni Shilingi 771 kwa kilo, wakati wastani wa bei ya juu ilikuwa ni Shilingi 1,612 kwa kilo. Miezi iliyokuwa na bei ya chini kuliko yote katika kipindi hicho ni Julai, Agosti, Octoba na Novemba 2022 pamoja na mwezi Juni 2023 kwa bei ya Shilingi 700 kwa kilo. Aidha, mwezi Desemba 2022 ulikuwa na bei ya juu kuliko miezi yote katika kipindi husika kwa bei ya Shilingi 1,890 kwa kilo. Hata hivyo, uchambuzi wa bei ya wastani ya mahindi nchini bila kujali bei ya chini au bei ya juu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikuwa ni Shilingi 1,200 kwa kilo.

## ii. Unga wa Mahindi

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Ugavi wa unga wa mahindi unaathiriwa moja kwa moja na upatikanaji wa mahindi makavu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 wastani wa bei ya chini ya unga wa mahindi ilikuwa ni Shilingi 1,283 kwa kilo, wakati wastani wa bei ya juu ilikuwa ni Shilingi 2,006 kwa kilo. Mwezi uliokuwa na bei ya chini kuliko yote katika kipindi hicho ni Julai 2022 kwa Shilingi 1,100 kwa kilo. Aidha, mwezi Aprili 2023 ulikuwa na bei ya juu kuliko miezi yote katika kipindi husika kwa bei ya Shilingi 2,175 kwa kilo. Uchambuzi unaoenesha kuwa bei ya wastani ya unga wa mahindi nchini kwa mwaka 2022/2023 (bila kujali bei ya chini au ya juu) ilikuwa ni Shilingi 1,733 kwa kilo.

### iii. Mchele

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Uzalishaji wa mchele kwa mwaka wa 2021/2022 ulikuwa ni takribani tani milioni 1.708 ikiwa ni pungufu kwa tani 980,000 ukilinganisha na uzalishaji wa mchele kwa mwaka 2020/2021. Hivyo, ni wazi kuwa ugavi wa mchele ulioingia sokoni kwa mwaka 2022/2023 uliathiriwa kwa kiasi kikubwa na upungufu huo wa uzalishaji, jambo lililochangia kupanda kwa bei ya mchele kwa kiasi kikubwa kama tulivyoshuhudia katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.

Katika kipindi hicho, wastani wa bei ya chini ya mchele ilikuwa ni Shilingi 2,208 kwa kilo, wakati wastani wa bei ya juu ilikuwa ni Shilingi 3,367 kwa kilo. Mwezi Julai 2022 ulikuwa na bei ya chini kuliko yote katika kipindi hicho kwa bei ya Shilingi 1,750 kwa kilo, wakati mwezi Oktoba 2022 ulikuwa na bei ya juu kuliko miezi yote kwa Shilingi 4,000 kwa kilo. Bei ya wastani ya mchele nchini bila kujali bei ya chini au ya juu kwa mwaka 2022/2023 ilikuwa ni Shilingi 2,705 kwa kilo.

### iv. Maharage

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Uzalishaji wa maharage na mazao jamii ya mikunde kwa mwaka 2021/2022 ulikuwa ni tani milioni 2.499 ukilinganisha na tani milioni 2.236 zilizozalishwa mwaka 2020/2021. Hata hivyo, mwaka 2022/2023 tulishuhudia bei ya maharage ikipanda kwa kiasi kikubwa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 wastani wa bei ya chini ya maharage nchini ilikuwa ni Shilingi 2,156 kwa kilo, wakati wastani wa bei ya juu ilikuwa ni Shilingi 3,533 kwa kilo. Mwezi Julai 2022 ulikuwa na bei ya chini ya maharage kuliko yote katika kipindi hicho kwa bei ya Shilingi 1,650 kwa kilo, wakati mwezi Oktoba na Novemba 2022 ilikuwa na bei ya juu ya maharage kuliko miezi yote kwa Shilingi 4,000 kwa kilo. Uchambuzi unaonesha kuwa bei ya wastani ya maharage katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 nchini bila kujali bei ya chini au ya juu ilikuwa ni Shilingi 2,837 kwa kilo.

**v. Unga wa ngano**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Uzalishaji wa ngano kwa mwaka 2021/2022 ulikuwa ni tani 62,000 pungufu kwa tani 8,000 ukilinganisha na uzalishaji wa mwaka 2020/2021. Kiasi hiki ni takribani asilimia 10 tu ya mahitaji ya ngano kwa ajili ya kuzalisha unga wa ngano nchini. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa nchi huagiza ngano kutoka nje ya nchi. Mwezi Juni 2023 umekuwa na bei ya chini kuliko yote ya unga wa ngano katika kipindi hicho kwa bei ya wastani wa Shilingi 2,089 kwa kilo, wakati mwezi Agosti 2022 ulikuwa na wastani wa bei ya juu kuliko yote kwa Shilingi 2,571 kwa kilo. Bei ya unga wa ngano kwa mwaka 2022/2023 iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na vita vinavyoendelea baina ya Urusi na Ukreini.

**vi. Viazi Mviringo**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Uzalishaji wa viazi (viazi mviringo na vitamu) kwa mwaka 2021/2022 ulikuwa ni tani milioni 1.715 ukilinganisha na tani milioni 1.626 zilizozalishwa katika mwaka 2020/2021. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 wastani wa bei ya chini ya viazi mviringo nchini ulikuwa ni Shilingi 800 kwa kilo, wakati wastani wa bei ya juu ulikuwa ni Shilingi 1,702 kwa kilo. Mwezi

Julai 2022 ulikuwa na bei ya chini ya viazi mviringo kuliko yote katika kipindi hicho kwa bei ya Shilingi 1,050 kwa kilo, wakati mwezi Septemba 2022 ulikuwa na wastani wa bei ya juu ya viazi mviriongo kuliko miezi yote kwa Shilingi 1,868 kwa kilo. Uchambuzi unaonesha kuwa bei ya watani ya viazi mviringo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 nchini bila kujali bei ya chini au ya juu ilikuwa ni Shilingi 1,369 kwa kilo.

### vii. Sukari

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Tanzania ina jumla ya viwanda vikubwa vitano (5) vya kuzalisha sukari. Viwanda hivyo ni TPC, Kagera Sugar, Kilombero Sugar, Mtibwa Sugar na Bakhresa Sugar.  kwa msimu wa mwaka 2022/2023 viwanda hivyo, vilizalisha kiasi cha tani **444,000** na kwa msimu wa **2023/2024** vinategemea kuzalisha kiasi cha tani **530,000**. Mahitaji kwa mwezi yanakadiliwa kuwa tani **38,000.**

Uzalishaji kwa msimu wa 2023/2024 ulitarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei 2023, hata hivyo uzalishaji huo haukuanza kwa wakati kutokana na changamoto ya mvua kunyesha kwa kipindi kirefu nchini.

Kwa sasa hali ya uzalishaji umeimarika na kwa siku viwanda vyote vinazalisha kiasi cha tani **2,500**. Hivyo kwa mwezi (Siku 30) vitazalisha kiasi cha tani **75,000**. Hivyo kuna ziada ya tani **37,000**.

Bei ya watani ya sukari nchini katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 ilikuwa ni Shilingi 2,849 kwa kilo. Wastani wa bei ya chini ya sukari katika kipindi hicho ilikuwa ni Shilingi 2,588 kwa kilo, huku miezi ya Julai na Agosti 2022 ikiwa na bei ya chini kuliko yote kwa Shilingi 2,400 kwa kilo. Aidha, wastani wa bei ya juu ya sukari ilikuwa ni Shilingi 3,084 kwa kilo, huku mwezi Aprili 2023 ukiwa na bei ya juu ya sukari kuliko miezi yote kwa Shilingi 3,300 kwa kilo.

### viii. Mafuta ya kupikia

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Hadi kufikia Juni, 2023 Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 771 vya kuzalisha mafuta ya kula, kati ya hivyo, 21 ni viwanda vikubwa na vya kati; na viwanda 750 ni vidogo. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 205,000 za mafuta ambapo tani 180,000 ni mafuta ya alizeti na tani 25,000 ni mafuta ya mawese na pamba. Aidha, mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni takribani tani 570,000 kwa mwaka, hivyo tunaagiza tani 365,000 ili kutosheleza mahitaji ya mafuta ya kupikia nchini. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Juni 2023 wastani wa bei ya mafuta ya alizeti ilikuwa ni Shilingi 6,398 kwa lita. Hata hivyo, wastani wa bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti ilikuwa ni Shilingi 4,542 kwa lita, wakati wastani wa bei ya juu ilikuwa ni Shilingi 8,396 kwa lita. Miezi ya Aprili, Mei na Juni 2023 ilikuwa na bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti kuliko miezi yote kwa Shilingi 4,000 kwa lita, wakati miezi ya Julai, Agosti na Septemba 2022 ilikuwa na bei ya juu ya Shilingi 9,000 kwa lita.

## 3. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

### i. Saruji

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Hadi kufikia Juni, 2023, Tanzania ina viwanda vya saruji vipatavyo 14 ambapo kati ya hivyo, viwanda 7 ni vikubwa (intergrated plant) na vilivyobakia vinazalisha saruji kutokana na clinker iliyozalishwa na viwanda hivyo saba. Takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2022, zinaonesha kuwa viwanda vya saruji nchini vinazalisha tani 10,850,000 za saruji kwa mwaka ambapo mahitaji ya ndani ya nchi ni tani 7,100,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 3,750,000 ambayo huuzwa katika soko la nje hususan katika nchi za Congo, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 uchambuzi uanonesha kuwa kwa wastani, saruji aina ya 32.5R iliuzwa kwa ya Shilingi 17,009 kwa mfuko wa kilo 50. Wastani wa bei ya chini ya saruji ya aina hiyo nchini kwa kipindi hicho ilikuwa ni Shilingi 14,203 huku mwezi Julai 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Shilingi 12,500 kwa mfuko wa kilo 50. Pia, wastani wa bei ya juu ya saruji ya aina hiyo ilikuwa ni Shilingi 22,923 kwa mfuko wa

kilo 50, mwezi Januari 2023 ukiwa na bei ya juu kuliko mieze yote kwa Shilingi 24,700 kwa mfuko wa kilo 50.

Kwa upande wa saruji ya aina ya 42.5R, uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka 2022/2023 wastani wa bei ulikuwa ni Shilingi 18,217 kwa mfuko wa kilo 50. Wastani wa bei ya chini katika kipindi hicho ulikuwa ni Shiling 14,917 kwa mfuko wa kilo 50 huku mwezi Julai 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Shilingi 13,500 kwa mfuko wa kilo 50. Aidha, wastani wa bei ya juu ilikuwa ni Shilingi 23,800 kwa mfuko wa kilo 50 na miezi ya Aprili, Mei na Juni 2023 ikiwa na bei ya juu kuliko miezi yote kwa Shilingi 24,500 kwa mfuko wa kilo 50.

ii. **Mabati**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Hadi kufikia Juni, 2023 Tanzania ina viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha mabati kuanzia hatua ya awali (intergrated) ambavyo ni ALAF na MMI Steel vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jumla ya tani 158,000 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 58,189 kwa mwaka sawa na asilimia 37 ya uwezo uliosimikwa. Sambamba na viwanda hivyo vikubwa, kuna viwanda vidogo zaidi ya 50 vya kukunja mabati kutokana na malighafi ya mabati yaliyokwisha kupakwa rangi na kuyakunja migongo.

Katika kipindi cha kuanzia Juai 2022 hadi Juni 2023 wastani wa bei ya mabati meupe geji 30 ilikuwa ni Shilingi 24,882 kwa bati. Hata hivyo, wastani wa bei ya chini ilikuwa ni Shilingi 21,908 kwa bati huku mwezi Septemba 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Shilingi 21,000 kwa bati. Wastani wa bei ya juu ya mabati meupe geji 30 katika kipindi hicho ilikuwa ni Shilingi 28,733 kwa bati huku mwezi Septemba 2022 ukiwa na bei ya bei ya juu kuliko miezi yote kwa Shilingi 32,500 kwa bati.

Kwa upande wa mabati meupe geji 28, uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 bei ya wastani ilikuwa ni Shilingi 35,218 kwa bati. Wastani wa bei ya chini katika kipindi hicho ilikuwa ni Shilingi 29,745 kwa bati, huku mwezi Januari 2023 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote katika kipindi hicho kwa Shilingi 28,000 kwa bati. Aidha, wastani wa bei ya juu katika mwaka 2022/2023 ulikuwa ni Shilingi 41,682 kwa bati, huku mwezi

Agosti 2022 ukiwa na bei ya juu kuliko miezi yote katika kipindi hicho kwa Shilingi 52,000 kwa bati.

iii. **Nondo**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022, matumizi ya bidhaa za chuma nchini yameongezeka kutoka tani 226,000 hadi kufikia tani 1,000,000 kwa mwaka, sawa na ongezeko la asilimia 303.54. Hadi Machi, 2023, nchi yetu ilikuwa na viwanda 25 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo vipo katika makundi mbalimbali yanayojumuisha bidhaa zikiwemo nondo, mabomba, misumari na seng'enge. Kati ya hivyo, Viwanda vya kuzalisha nondo ni 16 vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,082,700 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 750,000 kwa mwaka sawa na asilimia 69 ya uwezo uliosimikwa. Mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 550,336. Hivyo, uzalishaji huo wa ndani hutosheleza mahitaji yote ya ndani na ziada kiasi cha tani 199,664 huuzwa nje ya nchi.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Juni 2023, wastani wa bei ya nondo mm 10 nchini ilikuwa ni Shilingi 19,546 kwa nondo. Aidha, katika kipindi hicho, wastani wa bei ya chini ya nondo mm 10 ilikuwa ni Shilingi 16,613 kwa nondo, huku mwezi Octoba 2022 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Shilingi 11,250 kwa nondo ya mm 10. Pia, wastani ya bei ya juu ya nondo mm 10 katika kipindi hicho ulikuwa ni Sh. 23,072 kwa nondo, huku mwezi Septemba 2022 ukiwa na wastani wa bei ya juu kuliko miezi yote kwa Shilingi 25,500 kwa nondo ya mm 10.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Juni 2023, wastani wa bei ya nondo mm 12 nchini ilikuwa ni Shilingi 25,098 kwa nondo. Aidha, katika kipindi hicho, wastani wa bei ya chini ya nondo mm 12 ilikuwa ni Shilingi 22,088 kwa nondo, huku mwezi Juni 2023 ukiwa na bei ya chini kuliko miezi yote kwa Shilingi 16,000 kwa nondo ya mm 12. Pia, wastani ya bei ya juu ya nondo mm 12 katika kipindi hicho ulikuwa ni Sh. 28,042 kwa nondo, huku mwezi Agosti 2022 ukiwa na wastani wa bei ya juu kuliko miezi yote kwa Shilingi 31,500 kwa nondo ya mm 12.

## MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU NCHINI KWA MWEZI JULAI 2023

## 1. UTANGULIZI

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Sasa nijikite katika kutoa taarifa za mwenendo wa mazao na bidhaa muhimu nchini kwa mwezi Julai 2023.

## 2. MWENENDO WA BEI ZA MAZAO NA BIDHAA ZA VYAKULA

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

### i. Mahindi

Bei ya mahindi kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 665 na 1,500 kwa kilo. Bei ya juu ya mahindi imeshuka kwa asilimia 3.2 ambayo ni sawa na kushuka kwa shilingi 50 ikilinganishwa na bei ya mwezi Juni, 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 1,550 kwa kilo. Vilevile, bei ya chini ya mahindi imeshuka kwa asilimia 4.8 sawa na kushuka kwa Shilingi 33 ukilinganisha na bei ya chini ya mahindi ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 700 kwa kilo. Bei za chini ipo katika mkoa wa Ruvuma na bei ya juu imeonekana katika Mikoa ya Pwani, Mtwara na Kilimanjaro. Wastani wa bei ya mahindi nchini umeshuka kwa asilimia 0.8 kwa mwezi Julai 2023 ukilinganisha na wastani wa bei ya mahindi kwa mwezi Juni 2023.

### ii. Unga wa Mahindi

Bei ya Unga wa mahindi kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 1,200 na 2,000 kwa kilo. Bei ya juu ya unga wa mahindi imeshuka kwa asilimia 2.4 ambayo ni sawa na kushuka kwa shilingi 50 ikilinganishwa na bei ya unga wa mahindi ya mwezi Juni, 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 2,050 kwa kilo. Hata hivyo, bei ya chini ya unga wa mahindi kwa mwezi Julai, 2023 haijabadilika ukilinganisha na bei ya unga wa mahindi ya mwezi Juni, 2023. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Iringa na bei ya juu ipo katika mikoa ya Singida, Pwani, na Kilimanjaro. Wastani wa bei ya unga wa mahindi nchini umeshuka kwa asilimia 1.5 kwa mwezi Julai 2023 ukilinganisha na wastani wabei ya unga wa mahindi kwa mwezi Juni 2023.

### iii. Mchele

Bei ya mchele kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 2,000 na 3,400 kwa kilo. Bei ya juu ya mchele imeshuka kwa wastani wa asilimia 1.4 sawa na kupungua kwa Shilingi 50 ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa ni kati ya Shilingi 3,450 kwa kilo. Bei ya chini ya mchele imepungua kwa asilimia 9.1 sawa na kupungua kwa Shilingi 200 ikilinganishwa na bei ya chini ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 2,200 kwa kilo. Mikoa yenye bei ya chini ya mchele ni Katavi na Tabora, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Mtwara. Ukiangalia wastani wa bei ya mchele nchini, uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya mchele kwa mwezi Julai 2023 umepungua kwa asilimia 3.2 ukilinganisha na wastani wa bei ya mchele kwa mwezi Juni 2023.

### iv. Maharage

Bei ya maharage kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 1,925 na 3,350 kwa kilo. Bei ya juu imeshuka kwa asilimia 6.9 sawa na kupungua kwa shilingi 250 ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 3,600 kwa kilo. Halikadhalika, bei ya chini ya maharage imeshuka kwa asilimia 6.1 sawa na kushuka kwa Shilingi 125 ukilinganisha na bei ya chini ya maharage ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 2,050 kwa kilo. Bei ya chini inapatikana katika mkoa wa Songwe, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Mtwara. Uchambuzi wa wastani wa bei ya maharage nchini unaonesha kuwa wastani wa bei ya maharage kwa mwezi Julai 2023 umeshuka kwa asilimia 2.2 ukilinganisha na wastani wa bei kwa mwezi Juni 2023.

### v. Viazi Mviringo

Bei ya Viazi Mviringo kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 850 na 1,600 kwa kilo. Bei ya juu ya viazi mviringo imeshuka kwa asilimia 5.9 sawa na kupungua kwa shilingi 100 ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 1,700 kwa kilo. Hata hivyo, bei ya chini ya viazi mviringo kwa mwezi Julai 2023 haijabadilika ukilinganisha na bei ya chini ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 850 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Rukwa, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Songwe. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya viazi mviringo kwa mwezi Julai 2023

imeshuka kwa asilimia 4.4 ukilinganisha na wastani wa bei ya viazi mviringo kwa mwezi Juni 2023.

**vi. Unga wa Ngano**

Bei ya unga wa ngano kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 1,900 na 2,300 kwa kilo. Bei ya juu ya unga wa ngano kwa mwezi Julai 2023 imepungua kwa asilimia 4.2 sawa na kupungua kwa Shilingi 100 ukilinganisha na bei ya juu ya mwezi Juni 2023 iliyokuwa ni Shilingi 3,400 kwa kilo. Kwa upande mwingine, bei ya chini ya unga wa ngano haijaonesha mabadiliko yoyote ikilinganishwa na bei ya chini ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 1,900 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam na bei ya juu ipo katika Mikoa ya Singida. Hata hivyo, wastani wa bei ya unga wa ngano nchini kwa mwezi Julai 2023 umepungua kwa asilimia 4.4 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo nchini kwa mwezi Juni 2023.

**vii. Sukari**

Bei ya sukari kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 2,700 na 3,300 kwa kilo. Bei hii ni himilivu. Takwimu zinaonesha kuwa mwezi Juni 2023 sukari iliuzwa kati ya shilingi 2,650 mpaka Shilingi 3,133 kwa kilo. Kwa mwezi Julai, bei ya chini ipo katika mikoa ya Tanga, Singida na Songwe na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Ruvuma. Ni matumaini yangu kuwa bei hizi zitaendelea kushuka zaidi kwani viwanda vimeshaanza uzalishaji toka mwanzoni mwa mwezi Julai, 2023. Hali ya kuchelewa uzalishaji imesababishwa na kuendelea kunyesha kwa mvua za masika hadi mwishoni mwa mwezi Juni, 2023 kwenye maeneo mengi yanayolima miwa.

**viii. Mafuta ya Kupikia**

Bei ya mafuta ya kupikia ya Alizeti kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 4,000 na 7,500 kwa lita. Bei ya chini na bei ya juu ya mafuta ya kupikia ya Alizeti imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika ikilinganishwa na bei ya chini na bei ya juu ya mafuta ya kupikia ya alizeti ya mwezi Juni, 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 4,000 na 7,500 kwa lita. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti inapatikana katika mikoa ya Singida na Kilimanjaro, wakati bei ya juu inapatikana katika mkoa wa Mtwara. Hata hivyo, uchambuzi unaonesha wastani wa bei ya mafuta ya kupikia ya alizeti kwa mwezi Julai 2023 imeshuka kwa asilimia 5.8 ukilinganisha na wastani wa bei ya mafuta hayo kwa mwezi Juni 2023.

Aidha, bei ya mafuta ya kupikia ya mawese kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 3,500 na 7,000 kwa lita. Kama ilivyokuwa kwa mafuta ya kupikia ya alizeti, bei ya chini na bei ya juu ya mafuta ya kupikia ya mawese imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika ikilinganishwa na bei ya chini na bei ya juu ya mafuta hayo ya mwezi Juni, 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 3,500 na 7,000 kwa lita. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya mawese inapatikana katika mkoa wa Iringa, wakati bei ya juu ya mafuta hayo inapatikana katika mkoa wa Mwanza. Hata hivyo, uchambuzi unaonesha wastani wa bei ya mafuta ya kupikia ya mawese kwa mwezi Julai 2023 imeshuka kwa asilimia 0.7 ukilinganisha na wastani wa bei ya mafuta hayo kwa mwezi Juni 2023.

## 3. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

### i. Saruji

Bei ya saruji (aina ya 32.5) kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 14,125 na 23,250 kwa mfuko wa kilo 50. Bei ya juu ya saruji hiyo imeongezeka kwa asilimia 0.5 sawa na ongezeko la Shilingi 125 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa ni Shiling 23,125 kwa mfuko wa kilo 50. Vilevile, bei ya chini ya saruji imeongezeka kwa asilimia 4.6 sawa na ongezeko la Shilingi 625 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 13,500 kwa mfuko wa kilo 50. Mkoa wenye bei ya chini ni Tanga, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Kagera. Aidha, uchambuzi wa wastani wa bei ya saruji (aina ya 32.5) nchini unaonesha kuwa bei yake imepanda kwa asilimia 3.2 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Juni 2023.

Kwa upande wa saruji (aina ya 42.5), uchambuzi unaonesha kuwa bei kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 15,000 na 24,875 kwa mfuko wa kilo 50. Bei ya juu ya saruji hiyo imeongezeka kwa asilimia 1.5 sawa na ongezeko la Shilingi 375 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa ni Shiling 24,500 kwa mfuko wa kilo 50. Halikadhalika, bei ya chini ya saruji ya aina hii imeongezeka kwa asilimia 2.4 sawa na ongezeko la Shilingi 350 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya mwezi Juni 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 14,650 kwa mfuko wa kilo 50. Mkoa wenye bei ya chini ni Tanga, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Kagera. Aidha, uchambuzi wa wastani wa bei ya saruji (aina ya 42.5) nchini unaonesha kuwa

bei yake imepanda kwa asilimia 1.4 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Juni 2023.

### ii. Nondo

Bei ya nondo mm 10 kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 11,750 na 18,000. Bei hiyo imeonesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadiliko yoyote ya bei ya juu au bei ya chini ukilinganisha za bei ya mwezi Julai 2023 na mwezi Juni 2023. Bei za chini zipo katika mkoa wa Tabora na bei ya juu ipo katika mkoa wa Iringa.

Bei ya nondo mm 12 kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 22,000 na 28,000. Bei hiyo imeonesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadiliko yoyote ya bei ya juu au bei ya chini ukilinganisha bei za mwezi Julai 2023 na mwezi Juni 2023. Bei za chini zipo katika mkoa wa Dar es Salaam na bei ya juu ipo katika mikoa ya Rukwa na Katavi.

### iii. Bati

Bei ya bati nyeupe geji 30 kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 21,500 na 27,000. Bei hiyo imeonesha uhimilivu kwa kutokuwa na mabadiliko yoyote ya bei ya juu au bei ya chini ukilinganisha za bei ya mwezi Julai 2023 na mwezi Juni 2023. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Iringa wakati bei ya juu ipo katika Mikoa ya Manyara.

## 4. MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA NYINGINE

### i. Sabuni

Bei ya Sabuni aina ya Jamaa, White wash na MO kwa mwezi Julai 2023 ni kati ya Shilingi 2,800 na 3,900 kwa mche. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Arusha, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Kagera.

Bei ya Sabuni aina ya Takasa, kiboko na Kuku kwa mwezi Julai ni kati ya Shilingi 1,200 na 4,000 kwa mche. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Mara, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Kagera.

Bei ya Sabuni za Magadi kwa mwezi Julai ni kati ya Shilingi 1,000 na 3,200 kwa mche. Sabuni za magadi zipo aina mbili nazo ni miche myembamba na

miche minene. Bei ya chini ipo katika mikoa ya Katavi, Tabora na Morogoro, wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Kagera.

## 5. HITIMISHO

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Napenda kutoa rai kwa wazalishaji wa bidhaa zote za viwandani kuongeza jitihada za uzalishaji wa bidhaa kwa ubora unaohitajika sokoni na kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali nchini. Hatutovumilia kuona mzalishaji, msambazaji au muuzaji wa bidhaa yoyote ile akiongeza kiholela bei ya bidhaa yoyote ile bila sababu ya msingi. Niwaelekeze kupitia kwenu maafisa biashara wote Nchini waliopo kwenye Halmashauri zetu kuhakikisha wanasimamia ipasavyo eneo hili la bei za bidhaa, ni jukumu letu kuwalinda wazalishaji na walaji pia.

……………………………………………………………

**Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb)**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**

**Julai, 2023**